**University of Dar es Salaam**

**Library Repository** **https://libraryrepository.udsm.ac.tz**

Mwalimu J.K Nyerere Speeches and Statements

2001

# Kazi za Taasisi ya Mwalimu Nyerere

Nyerere, Julius Kambarage

Taasisi ya Mwalimu Nyerere

Nyerere, J.K (2001),Kazi za Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Taasisi ya Mwalimu Nyerere,Dar es Salaam. p.35

http://41.86.178.5:8080/xmlui/handle/123456789/7042

*Downloaded from University of Dar es Salaam Library Repository*

EAF PAM
JQ3516
.T34T3



# Kazi za Taasisi ya Mwalimu Nyerere

TAASISI YA MWALIMU NYERERE

# Kazi za Taasisi ya Mwalimu Nyerere

LIBRARY ✲ UNIV. OF DAR ES SALAAM ✲
DB

# Kazi za Taasisi ya Mwalimu Nyerere

**Taasisi ya Mwalimu Nyerere**

6 Sokoine Drive, S. L. P. 71000, Dar es Salaam, Tanzania.

Kimechapishwa na: *Mkuki na Nyota Publishers, Mt. Muhonda, Na 6, Mission Quarter, Kariakoo, S. L. P. 4246, Dar es Salaam, Tanzania,*
www.mkukinanyota.com

kwa niaba ya: *Taasisi ya Mwalimu Nyerere, 6 Sokoine Drive, S. L. P. 71000, Dar es Salaam, Tanzania.*

© Taasisi ya Mwalimu Nyerere, 2001

**ISBN 9987 686 80 - X**

Maandishi haya yanaweza kunukuliwa bila sherti la kuwasiliana na Taasisi ya Mwalimu Nyerere ila hairuhusiwi kuyachapisha kwa ujumla wake katika matoleo ya kibiashara kwa njia yo yote, kwa kuyachapa au kuyaweka kwenye mtandao wa kielektroni bila ruhusa maalumu kwa maandiko kutoka Taasisi ya Mwalimu Nyerere au Mchapishaji.

Printed & Supplied by Rainbow International, New Delhi (India).

# Yaliyomo

SEHEMU YA KWANZA .......... 1

Maelezo ya Mwalimu .......... 1
Mwanzo wa Tume ya Kusini (South Commission) 1986 .......... 1
Safari za Kutafuta Maoni ya Wengine na Uthibitisho wa Kuelewa Kwao .......... 2
Mwanzo wa South-Centre - Geneva .......... 3
Ufafanuzi wa Kazi za Taasisi ya Mwalimu Nyerere (The Mwalimu Nyerere Foundation) .......... 4
Umuhimu wa Umoja .......... 4
Umuhimu wa Ukubwa wa Soko .......... 5

SEHEMU YA PILI .......... 7

Maswali na Majibu .......... 7
Kwa Nini South Centre Iko Geneva .......... 10

SEHEMU YA TATU .......... 33

Waziri Mkuu .......... 33

# SEHEMU YA KWANZA

## Maelezo ya Mwalimu

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge. Mimi vilevile nianze kwa kuwashukuruni kwa kunipa nafasi hii ya kuelezea kama nilivyoombwa na wenzangu kitu hiki kinachoitwa Mwalimu Nyerere 'Foundation', wanaita Shirika. Mimi hofu yangu, nadhani ukiiita Shirika watu watafikiri mna mapesa chungu nzima au mnafanya biashara; mtapata taabu sana. Kwa hiyo mimi naona afadhali mtafute jina lingine au kama hamtapata kabisa afadhali muiite Taasisi. Kazi waliyoomba nifanye ni kueleza kazi ya Shirika lao hilo, za Foundation kwa Kiingereza. Nilifikiri nieleze shughuli za nyuma kidogo.

Labda nieleze kidogo shughuli nilizokuwa nazifanya miaka hii ya nyuma, kwa sababu nikieleza hivyo itakuwa rahisi kidogo kuelewa kwa nini wamependekeza tuanzishe Foundation hii. Baadhi yenu mnafahamu vizuri, baadhi mnaelewa kidogo, kwamba baada ya kung'atuka (Novemba 1985), mwaka 1986 nilijishughulisha na kazi ya Chama. Mwaka huo wa kwanza baada ya kung'atuka nilishughulika kidogo na kazi za Chama. Wabunge hapa mnisamehe, wakati huo tulikuwa bado tuko nyuma sana: hatujaendelea; tulikuwa na chama kimoja tu! Niliombwa na wenzangu wa Chama kuwasaidia shughuli za Chama chao. Kwa hiyo, mwaka 1986 kwa kweli nilishughulika kufanya kazi zao.

## Mwanzo wa Tume ya Kusini (South Commission) 1986

Kabla ya mwisho wa mwaka ule 1986, baadhi ya Viongozi wa Nchi za Kusini waliniomba nianzishe Tume ya kufanya uchambuzi wa kina kidogo juu ya maendeleo ya nchi zetu za Kusini tangu miaka 30 iliyopita na kuweza kuona tumefanya nini katika miaka hiyo, tumefanya maendeleo gani, na tumepata matatizo gani; na kutokana na uchambuzi huo Tume iweze kufanya mapendekezo fulani kwa kipindi kinachofuata. Nikakubali. Mwezi wa Septemba 1986, nikaanza shughuli ya kutembeatembea katika maeneo hayo, nikatembelea nchi nyingi kidogo; nchi 19 katika Asia na Latin Amerika kuanza kueleza hivyo: kazi niliyoombwa kuifanya.

## Safari za Kutafuta Maoni ya Wengine na Uthibitisho wa Kuelewa Kwao

Pamoja na nchi zenyewe kukutana Harare katika mkutano wa NAM[1], sikuwa na uhakika kama wamelikubali jambo lenyewe, wameelewa vizuri au walilielewa juujuu tu kwa sababu ni wachache miongoni mwao ambao walikuwa na wazo hili. Kwa hiyo, nikaona nitembelee baadhi ya nchi nihakikishe hii kazi wanayotaka niifanye wanaielewaje; vilevile niweze kuzungumza na watu ambao watateuliwa kuingia katika Tume hiyo. Kazi hiyo nikaifanya mwaka 1987 miezi ya mwanzo. Kufika Oktoba 1987 nikaanzisha Tume.

Tume hiyo ikafanya kazi kwa miaka mitatu, tukatoa Ripoti. Ripoti ile inapendekeza kwamba Nchi za Kusini zifanye maendeleo, maendeleo yenyewe yatokane na yalenge watu. Kwamba Nchi za Kusini inafaa ziwe na mshikamano kama zinataka kukabiliana na Nchi za Kaskazini kwa sababu zina uwezo mkubwa zaidi. Nchi za Kusini vilevile zishirikiane; hazina utaratibu wa kushirikiana kwa biashara. Nyingi ya nchi hizo zina mazoea ya kufanya biashara na Nchi za Kaskazini lakini hakuna utaratibu mzuri wa Nchi za Kusini kufanyiana biashara wenyewe kwa wenyewe au hata katika uwekezaji rasilimali. Nchi za Kusini zimekuwa na uwezo wa kuwekeza rasilimali lakini zinapeleka pesa zao katika Nchi za Kaskazini. Ziko pesa nyingi zinazotoka Kusini. Zinafanya kazi Kaskazini. Wataalamu wengi wako Kusini lakini nchi za Kusini zinatafuta wataalamu, badala ya kuwatafuta Kusini wanakwenda Kaskazini. Wataalamu wanahama katika nchi zetu wanakwenda Kaskazini – aliyenacho atapewa na asiyenacho atanyang'anywa hata kile kidogo alichonacho. Tunashauri nchi hizi kushirikiana. Hayo ndiyo yaliyokuwa mapendekezo yetu. Na kushirikiana kwa nchi hizo zishirikiane katika ngazi ya Afrika nzima, lakini pia Afrika, Asia, Latin Amerika washirikiane; makundi yashirikiane. Shughuli hizi zinafanyika, baadhi ya nchi zimekazana. Huko Asia, nchi ambazo zina maendeleo ni zile zinazoshirikiana.

---

[1] NAM: "Non Aligned Movement"

## Mwanzo wa South-Centre - Geneva

Tulipomaliza kazi hiyo, wenzangu wakaniomba ofisi yetu ya Geneva, Sekretariati ile iliyohudumia Tume, tuipunguze kidogo, iendelee kwa miaka 2, iitwe 'Centre' na mimi niitumie ile kwa miaka miwili nielezee shughuli za maamuzi na mapendekezo ya Tume. Nitembee tena tuone kama wameyaelewa na wale wanaotaka kuyatekeleza tuwasaidie wafanye hivyo. Baada ya hapo niifunge ofisi ile. Nikaifanya kazi hiyo, 1991. Mwaka1992 nikaenda Brazil kwenye mkutano wa Maendeleo na Mazingira, mwezi Juni. Na kutoka kule nikadhani ili kurahisisha zaidi kazi na kupunguza gharama, nikawaita (Makamishina) wenzangu waje Geneva niwaeleze kazi niliyoifanya na kwamba Oktoba 1992 nitaifunga ofisi kama tulivyokubaliana. Nikawaita, wakaja tukazungumza wakasema huwezi kufunga ofisi. Hii Centre sasa badala ya kuwa Centre tu ya miaka miwili, jaribu kuifanya iwe ni Centre ya kudumu. Wakanipa kazi ya kuanzisha Centre ya kudumu. Baadhi ya nchi pia ziliniambia kwamba hakuna haja ya kuifunga Centre. Vuguvugu la Nchi zisizofungamana na nchi za 'Group of 77' hazina chombo cha kuwasaidia; hakuna mahala ambapo inatoka sauti ya Nchi za Kusini.

Nikahangaika na kazi ile ya kuanzisha Centre ya kudumu. Ikachukua miaka miwili na tukaanzisha Centre ya kudumu. Centre ilikuwa inajitegemea. Centre ya sasa ni chombo cha Serikali sio chombo cha kiraia (Asasi Isiyokuwa ya Serikali) ni Oganizesheni ya serikali zihusikazo, na tulifanya hivyo ili ipate kutambuliwa kidiplomasia, pale Geneva. Nchi zilizotia sahihi mkataba ni kama 49 pamoja na nchi zile kubwa kubwa India, Brazil, Afrika ya Kusini na kadhaika. Katika mkataba tumeizuia Centre kuwa 'Sekretariati' ya Serikali za Nchi za Kusini. Kisheria ni Centre ya kiserikali lakini katika mkataba tumeizuia kuwa Sekretariati ya kiserikali: maana hatutaki kuwa na chombo kinachotumiwa na Serikali kwa maamuzi ya Serikali kwa sababu kitashindwa kutoa maamuzi kama wanavyoona wataalamu. Itakuwa Kenya inasema nini, Tanzania inasema nini. Na kwa nchi, mara nyingi huwa hazielewani. Ili kuwe na manufaa tuliamua tuiache Centre iwe huru, iwe inatoa maamuzi bila kuingiliwa na serikali.

## Ufafanuzi wa Kazi za Taasisi ya Mwalimu Nyerere (The Mwalimu Nyerere Foundation)

Tumekuwa na mawazo ya kuanzisha kachombo kengine kadogo – ka-Foundation kadogo. Mimi nikafikiri ni vyema tukaanzishe kaFoundation kadogo kasiwe ka kufanya kazi hiyo kwa Nchi za Kusini lakini kafanye kazi kwa nchi za Afrika. Sio kazi yake tena kaFoundation hako kama South Centre ambayo inafanya kazi kwa nchi zote za Kusini, bali kashughulike na mambo hayo hayo lakini kwa eneo na mambo ya Afrika sio nje ya Afrika. Kazi inayofanywa na South Centre kwa nchi zote za Kusini ifanywe na Foundation kwa nchi za Afrika peke yake. Hiyo kazi moja: Maendeleo ya watu. Lakini kabla ya hapo tulikuwa na kazi nyingine moja hiyo ya jitihada za awali za maendeleo; ilikuwa ni jitihada ya kushirikiana.

## Umuhimu wa Umoja

Mimi bado ni muumini kwamba vi-nchi vyenu hivi ni vidogo mno; mkiendelea navyo hamuendi mbali. Lazima mjitahidi kuziunganisha nchi zetu. Rais Clinton wa Marikani nasikia aliwahi kuulizwa na wanafunzi; kuwa WaChina hawa hawaheshimu haki za binadamu lakini Marikani mnang'ang'ania biashara nao kwa nini? Akawajibu wanafunzi hao: tunapofanya biashara na Wachina, Wachina wanauza vitu kwetu na vinatakiwa, na Marikani wanavinunua kwa faida yao wenyewe na wanauza kwa faida yao wenyewe. Ni kitu cha faida kwa Marikani. Uchina ni nchi kubwa, inatazamiwa kwamba ifikapo mwaka 2025 itakuwa ni Taifa Baba kwa Uchumi Duniani (nchi ya uchumi kambambe kuliko zote duniani). Clinton anasema hivyo juu ya Uchina. China ni nchi maskini lakini ni kubwa. Hivi sasa soko la Uchina ni kubwa sana pamoja na kwamba wastani wa pato la kila mchina ni dogo na haliingii hata robo ya Marikani, lakini uwezo wa soko lake ni kubwa sana kwa sababu ni nchi kubwa. Afrika ya Kusini wastani wa pato kwa kila mtu (pato la wastani la mtu) ni zaidi ya mara tatu ya China, lakini Afrika ya Kusini ni soko kwa nani? Namibia ni sawa na China lakini nani anawaza sana soko la Namibia; nchi ni ndogo sana, unaweza kuisahau. Tanzania yenu hivyo hivyo tu; nani anafikiria sana soko la Tanzania. Dunia inayokuja si dunia ya huruma

na si dunia ya mchezomchezo. Watu wanafikiri dunia inayokuja ni ya mchezomchezo; kutakuwa na mashindano ya teknolojia na mashindano ya uchumi ya ajabu kabisa kwa sababu tunaingia katika dunia nyingine kabisa. Mashindano yake yatakuwa ni makali sana, hivyo lazima mjenge nguvu. ViTanzania hivi, viKenya hivi viZimbabwe peke yao havina nafasi katika dunia hiyo. Wazungu wanaona hivyo, wakubwa wazito wanatambua hivyo. Pato la wastani kwa mtu wa Ubelgiji ni sawa sawa na la Afrika yote Kusini mwa Sahara ukiondoa Afrika ya Kusini.

## Umuhimu wa Ukubwa wa Soko

Ubelgiji ina watu milioni 10 lakini mapato yake kwa mwaka ni sawa na mapato ya Waafrika milioni 470 wanaoishi Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukiondoa Afrika ya Kusini. Hamna matumaini ya siku zijazo! Mkikaa hivi mnafikiri mchezo, hakuna matumaini huko tuendako. Kazi yetu wazee ni kuwaambieni mjiandae huko mbele ya safari, hakutakuwa na lelemama tuendako. Hakuna lelemama huko, kwa hiyo kitu kimoja ambacho daima nimekuwa nikifikiria, na kusema, na jinsi miaka inavyoendelea naimarisha imani yangu ni kuwa hakuna hatma nzuri ila katika umoja, katika Afrika hii. Afrika haina matumaini ya lolote isipojenga na kuimarisha *umoja* wake. ViRwanda, viBurundi vikibaki peke yao hivi vitafikiria Wahutu, Watutsi, Wahutu, Watutsi! – lazima kufikiri zaidi ya hapo. Ulaya na ukubwa wao wote ule, kaBelgium kale, hali yake ni hiyo ukilinganisha na Afrika. Lakini yapo mataifa makubwa; Ujerumani, na wengine wote; lakini wanajiona wadogo sana huko tuendako kupambana na Marikani, Uchina, India, kwa hiyo wanaungana. Ziko nchi za kizamani kama Uingereza bado zina maoni ya siku za nyuma. Wanaambiwa lazima muungane na wengine, wanasita. Uingereza pale, wenye akili wanaona hawana hatma bila kuungana na Wazungu wengine wa Ulaya. Hao ndio wakubwa wetu ambao wametutawala na ambao hatuwasogelei hata kidogo kwa tekinolojia wala soko, wala kwa chochote. Hayo ndiyo maoni yao; kuungana. Afrika mnataka mrudi kwenye ukabila, au mving'ang'anie vi-nchi vyenu hivi.

Mimi maoni yangu tangu zamani ni hayohayo na sasa ninaamini hata kushinda hapo awali kwamba ni lazima tuendelee kuhubiri *umoja* na

tujenge umoja na tuutumie umoja kushindana na wengine katika dunia ijayo.

Nilipenda kaFoundation hako kaendeleze kazi hiyo – kuhubiri umoja wa Afrika - kazi ya pili ya kaFoundation hako ni Afrika. Lakini umoja na wala maendeleo hayawezekani bila *amani*. Kwa hili sina haja ya kulisema sana, kwa hiyo tunataka kazi ya tatu, kaFoundation kashughulike na *Amani* katika Afrika. Amani baina ya nchi na nchi na amani ndani ya nchi.

Zamani matatizo ya amani yalikuwa ni ya nchi na nchi zinapigana, na hili bado katika Afrika lipo, nchi na nchi zinapigana. Lakini duniani inaelekea magomvi baina ya nchi na nchi yatazidi kuwa yanapungua hasa kwa nchi kubwa; yanapungua kwa sababu wanaogopana kwa sababu ya silaha walizonazo, wanaogopa wanaweza kumalizana. Eti kutazamia kwamba kesho na kesho kutwa Wamarikani watapigana na Warusi ni ngumu sana kwa sababu vita vya sasa si vya zamani. Vita vya zamani wewe unayeamua ulikuwa hufi. Vita vya sasa ukiamua vita wewe unakufa na wengine watakufa. Kwa sababu wewe utabonyeza silaha za nyuklia zilipuke na mwenzio naye atabonyeza. Wale waamuzi kwamba vifanyike hawaamui vifanyike baina yao; wanaweza kuamua vifanyike baina ya Tanzania na jirani yake lakini hawaamui vifanyike baina ya wao kwa wao. Kwa hiyo, vita baina ya nchi na nchi hasa nchi kubwa havitakuwepo; labda nchi zetu hizi kwa kusukumwa na wakubwa kwa faida zao wenyewe lakini kubwa zaidi itakuwa ni vita ndani ya nchi. Wenyewe kwa wenyewe; Rwanda, Burundi, Msumbiji, Angola, Somalia. Matatizo ya kutokuwapo kwa amani yatakuwapo ndani ya nchi; wenyewe kwa wenyewe. Dawa yake ni *maendeleo* na *umoja, kushirikiana*. Tunataka kaFoundation hako kashughulike na kazi hiyo: *amani katika Afrika, maendeleo katika Afrika* na *Umoja katika Afrika*.

Zamani, Waheshimiwa, ningemaliza kwa kusema 'Kidumu Chama cha Mapinduzi'!

# SEHEMU YA PILI

## MASWALI NA MAJIBU

**Mheshimiwa Jackson Makweta, Mbunge** *aliuliza juu ya Umoja wa Nchi za Afrika.*

**Mwalimu:** Kwame Nkrumah na mimi tulikuwa tunahimiza umoja wa Afrika. Kwame alikuwa na haraka zaidi aliona eti mnaunganisha nchi mbili hapa, tatu pale, akasema ile ni kuendelea kuunda vinchi vidogo vidogo. Yeye alitaka mkutane muunganishe nchi. Nikasema kwamba mimi sidhani kwamba hili litawezekana kwa sababu hatuwezi kupata 'Napoleon' mmoja akazipiga nchi zote hizi akaziweka pamoja; hata 'Napoleon' angeshindwa. Kwame angalikuwepo leo angaliweza kuniambia; sasa Mwalimu njia yako imefaulu? Lakini ni kweli haijaondoa haja ya kuendelea kufanya jitihada kuleta umoja. Maana inawezekana sisi wakati ule tulikuwa tumeona lakini hatukuwa na matatizo; ninyi mnayaona vizuri zaidi matatizo ya kutokuungana. Kwa kweli ni vizuri mfanye jitihada, sio sisi tena. Ninyi mnayaona zaidi kuliko sisi, sisi tulijaribu tukafika hapo tulipofika. Shabaha yetu ilikuwa ukombozi na umoja, ukombozi tulifaulu. Umoja tumefika hapo tulipofika lakini na nyinyi mchukue hapo tulipofika muuendeleze. Na ninyi mfike hapo mtakapofika, lakini msiache eti kwa sababu ni jambo gumu.

Ndugu Makweta alikuwa pia na maoni juu ya matatizo haya; yanatokana na nani! Mwenyewe anaona yanatokana na matatizo yetu ya uongozi mbovumbovu katika nchi zetu, na dhana ya demokrasia na nini kianze; uchumi uanze au demokrasia ianze.

Mimi sidhani kwamba katika jambo hili la demokrasia itakuwa kufikiri kuwa eti mngoje mpaka mtakapokuwa matajiri ndio muwe na demokrasia sidhani inawezekana. Au itakuwa ni hadithi ya Magiriki ya kuvuka mto: mtoto hataki kuvuka mto; anaulizwa anangoja nini kuvuka mto, anasema anangoja kwanza maji yapite! Nadhani tunahangaika na demokrasia ya umaskini na tutazijua mbinu zake. Tanzania mmefaulu – hii hapa, kikao

chenu hiki Bungeni, ndio demokrasia yenyewe. Watu wakiwa wana nia ya kufaulu wanafaulu.

**Mheshimiwa Dk. Aman Walid Kabourou, Mbunge** *kanikumbusha historia kidogo kwamba nilikuwa nikienda Burundi na kuonana na kiongozi wa Burundi wakati ule.*

**Mwalimu:** Mara yangu ya kwanza kwenda Burundi ilikuwa mwaka 1957 nikitoka kwenye uhuru wa Ghana nikapita Bujumbura. Tukazungumza na kiongozi wa pale jamaa mmoja aliyeitwa Rwagasore – Prince Rwagasore. Juzi tarehe 18 wiki moja kabla Buyoya hajatwaa madaraka nilipata bahati nikapata kajukuu ka kiume nikakaita Rwagasore. Nilionana na Rwagasore pale; nilikuwa natoka Ghana kwenye Uhuru na wakati huo TANU inaanzishwa na imeanza na shamrashamra kidogo Kigoma, tulikuwa na kamotomoto kidogo pale. Nilipokuwa Umoja wa Mataifa 1955, balozi wa UN wa Ubelgiji alinipiga maswali mengi kidogo pale ya kunisumbuasumbua. Basi nikaona niende Bujumbura na nikaonana na Rwagasore tukazungumzazungumza na baadaye akaanzisha UPRONA. Ni kweli vyama vile UPRONA na TANU vilishirikiana sana, baadhi ya wanachama wa TANU walikuwa na kadi za UPRONA na wanachama wa UPRONA walikuwa na kadi za TANU. Na kama anavyosema yule mama ilikuwa vigumu kujua nani ni nani. Kigoma ilikuwa vigumu kujua nani Mrundi na nani Muha tu wa kawaida, kwa sababu Waha na Wahutu ni walewale. Na si Waha tu ni walewale, na hata watawala wao ni wal wale. Juzijuzi nilipokuwa nazungumza habari za Mwami Ntare walidhani kwamba nazungumza habari za Mwami Ntare wa kwao. Nikawaambia hapana, Mwami Ntare wa kwetu. Hawa ni watu walewale. Tulishirikiana sana, na Rwagasore alijenga chama cha UPRONA; kile kilikuwa chama kinachofanana kabisa na TANU. Kilikuwa ni chama cha Warundi wote. Na katika uchaguzi wao wa kwanza kabisa kabla ya Uhuru walishinda na ni kwa sababu Wahutu ni wengi. Bunge lilikuwa la Wahutu wengi kuliko Watutsi na Waziri Mkuu alikuwa Mhutu na Rwagasore alikuwa ni mtu ambaye hajali – alikuwa Mtutsi na mkewe alikuwa Mhutu lakini alikuwa hajali mambo ya ukabila. Lakini Wabelgiji hawakumpenda kwa sababu alikuwa mpenda maendeleo

kidogo. Hawakumpenda kwa sababu walidhani atakuwa Lumumba mwingine. Burundi ina sehemu mbili za safu ya juu ya ukabila. Tabaka mbili, ya juu ile ina sehemu mbili ya utawala ina wale Abezi wa Kaskazini; kina Rwagasore walitokana na hawa wa Kaskazini. Wahima wa Kusini hawa walikuwa kama wanadharauliwa kidogo kwa hiyo Wabelgiji walipoona kwamba Abezi hawa wanaanza kufanya fujo walidhani huyu atakuwa Lumumba mwingine wakawashawishi Wahima nao waanzishe chama.

Wakaanzisha chama kingine na Wabelgiji wakashirikana na chama hicho kidogo kumuua Rwagasore. Kwa hiyo, Micombero ni Mhima akamtoa Mwambutsa wakaanzisha Jamhuri na tangu hapo ni Wahima wa Burundi ndio wanaotawala. Kuanzia hapo wakaanza kukivuruga chama. Bunge la Rwagasore lilikuwa la Wahutu na Watutsi lakini Wahutu wengi zaidi. Jeshi lilikuwa na Wahutu na Watutsi lakini Wahutu wengi zaidi maana ndio kawaida. Lakini baada ya hapo akina Micombero wakaanza kubadili, na chama taratibutaratibu kikawa cha Watutsi na jeshi likawa la Watutsi. Micombero ameendelea pale akatolewa na Bagaza, binamu yake wa Bururi palepale na Bagaza akatolewa na Buyoya, binamu yao wa Bururi palepale. Ni jamaa hawa: ni Watutsi wa Bururi. Jambo la kusema Watutsi, Watutsi si zuri sana ni ujinga mtupu. Ni Watutsi wa Bururi na wala wanaofaidika si Watutsi wote ila ni hao wachache, kakikundi kamoja haka. Mauaji yakianza ni Watutsi wanaouawa na wanatelekezwa na hawa wa Bururi. Hivyo ndivyo ilivyokuwa.

Ni kweli pale Burundi na hasa Bujumbura wapo wageni, na kama Kigoma pale kuna mchanganyiko wa makabila. Hata Bujumbura kuna mchanganyiko mkubwa sana. Ukizungumza na Waswahili pale Kiswahili chao ni sawa na cha watu wa Ujiji. Ni kweli kuna Waswahili hawa wageni; tatizo lipo na litagusa wanaotoka nje. Suala la kwamba watapata haki pale wakati wenyewe Wahutu na Watutsi wana tatizo basi wageni kama Watanzania walio pale hawawezi kuzungumza kabisa. Kwa hiyo, kimsingi tatizo lipo, kimsingi ni lao nyumbani na litawagusa na wale wanaotoka sehemu zingine. Hata wao watazungumza habari za wazawa, na wazawa ni wazawa wa Burundi!

## Kwa Nini South Centre Iko Geneva

Tumeifikiria sana; ni 'South Centre' na kwa kweli ingekuwa vizuri zaidi ikawa katika mji mkuu wa moja ya nchi zetu za Kusini. Sababu moja ni ya kihistoria. Tulipoanzisha Tume, ilikuwa ni Tume ya muda, tukafikiria tuiweke wapi? Tungeiweka katika nchi fulani ya Kusini; ziko siasa zake na kwa sababu ni Tume ya miaka mitatu tu na tunataka habari, pale Geneva ni mahali pazuri sana pa kupata habari. Unaposema Umoja wa Mataifa watu wanafikiria New York. Pale New York hakuna kitu sana; ni kitengo cha siasa, lakini vyombo vyote vikubwa vya UN viko Geneva: WHO, UNHCR, UNCTAD, WTO, WIPO. Vyombo karibu vyote vikubwa vya Umoja wa Mataifa viko pale; ni Centre ya Habari. Kwa hiyo tulienda pale kwa sababu hiyo – ni Centre ya habari. Ukitaka 'information' zote ziko pale. Ndio tumeenda hivyo mpaka wakasema sasa Mwalimu anzisha Oganizesheni ya Serikali zinazohusika.

Oganizesheni ya Serikali zinazohusika iko pale halafu uanze kufikiria kuipeleka Kusini; utaingiza siasa. Hasa kuipeleka Kusini, Kusini wapi? Ukitaka uipeleke Kusini ziko siasa za Kusini na mwamuzi nani; ni mimi, inakuwa ngumu sana. Na kwa kujua hivyo, vilevile kuibakiza pale, ina manufaa. Tunayo Centre nyingine New Delhi, imeanzishwa na NAM[1] - iko New Delhi. Huisikii, imeanzishwa na NAM, iko New Delhi haisikiki kabisa kabisa kwa sababu inahusishwa na India. Hata wakitayarisha makala nzuri sana, wanaihusisha na India; wanaisahau wanaona haina maana. Ipo faida ya kuwa Geneva kwa sababu inasaidia kutohusishwa na nchi yoyote – 'South Centre' iko pale, basi! Kwa sababu haiko katika nchi moja ya Kusini basi siasa hizi za wivuwivu hakuna. Kwa hiyo tukitoa makala pale ni ya South Centre. Ingekuwa New Delhi ingedhaniwa kwamba ni ya India au tungekuwa Beijing wangesema mambo ya Wachina kumbe si ya Wachina ni South Centre! Kwa hiyo tumeona ni vizuri ikae pale, haina matatizo.

**Mheshimiwa Mateo Qaresi, Mbunge** *alitaka kujua ikiwa viongozi wetu waliofanya uamuzi wa kuiwekea Burundi vikwazo wana umoja.*

**Mwalimu:** Nafurahi sana umeuliza swali hili. Yako mambo yanayozungumzwa, mimi nimekaa nao hawa viongozi wa Burundi na

najua msimamo wao. Baada ya 'Arusha I' tulipokuwa tunazungumza habari ya Burundi, Serikali ya Rais Ntibantunganya walikuja wakaomba kama nchi hizi zinaweza kuwapelekea msaada wa majeshi. Maombi yale yakakubaliwa na viongozi wale waliokutana Arusha katika kikao chao kile cha kwanza. Baadaye watu wakadhani kwamba labda Kenya haimo, haiwezi. Ilikuwa haimo kwa maana kwamba si nchi zote zilizokubaliana kupeleka msaada wa kijeshi pale. Kwa mfano Rwanda walisema 'hatuwezi: kwa sababu sisi tunaonwa na baadhi ya watu wa Burundi kwamba sisi ni sehemu ya tatizo. Rais Moi hakusudii kupeleka majeshi, Tanzania, Uganda, Ethiopia walikuwa tayari, Zaire sina hakika. Wahutu walikuwa na mashaka na Waganda kwa sababu Waganda wanawezaje kuingiza majeshi hapa na wao ni Watutsi (Museveni)? Halafu katika hili la juzi la vikwazo; Uganda nao watakubali? Walizungumza kwamba pengine Kenya, Uganda, Rwanda hawatakubali vikwazo, na Zaire, ikabaki Tanzania.

Maoni haya hayana msingi hata kidogo. Mimi nakaa nao, nazungumza nao; kwanza, niliowaomba waje Mwanza nilipopata matatizo Mwanza II, ni Rais wetu na Rais Museveni. Wakaja, nikawaeleza. Msimamo wao ni uleule na kama ungewaweka katika mizani wawili hawa mmoja ambaye ana msimamo mkali zaidi ni Rais Museveni. Na hili napenda mlikubali kwa sababu ukweli unasaidia katika kuendeleza shabaha mnayotaka, uongo unavuruga tu. Mkikubali ukweli mtasaidia. Kuanza kumshuku Rais Museveni, hasa ninyi hapa, atashangaa kabisa. Ataona Watanzania hawa wanaota kasumba gani hawa? Atasema: nakaa naye Mwalimu, Rais Mkapa nakaa naye, tunaelewana waziwazi kabisa halafu wao wanakwenda kule wanawaambia nini Watanzania wenzao? Na sisi tunakubaliana na msimamo wa Rais Museveni kabisakabisa. Na sasa hili la vikwazo: Rais Museveni alikuwa haamini vikwazo kwamba vitafanya kazi maana wengine kama Kimbau hapa mmekuwa mkisema vikwazo hivi; kwa nini tusiingie mara moja Burundi na kumaliza mambo. Rais Museveni tumekuwa tukimshawishi akubali vikwazo si kwa maana kwamba alikuwa hakubali lakini kwa maana kwamba havitafanya kazi. Sasa tunamwambia hapana mambo haya ya kutaka kuingiza majeshi pale ni magumu na inataka msaada wa mataifa makubwa yaweze kulipia majeshi haya tukiyapata.

Ni rahisi zaidi kutumia vikwazo, nchi zinazoumia ni Tanzania, Kenya, Uganḍa na Rwanda ndio hasa zinazohusika. Lakini bado nchi za wakubwa zinanung'unika. Lakini hatuombi msaada mkubwa zaidi kama ingekuwa ni kuingiza majeshi. Upo urahisi wa kuweka vikwazo na ukapata msaada wa kimataifa kuliko majeshi – ukapata msaada wa majeshi na ukapata msaada wa kimataifa hata kama ni kulipia tu. Kwa hiyo tukakubali. Ninawaelezeni vizuri ili mjue, nadhani jambo hili ni muhimu kabisa. Iko ile taarifa ya pamoja. Ina vipengele vyake fulanifulani ibara ya 7 ya taarifa ya pamoja ile inasema "Mkutano wa viongozi wakuu wa Eneo unataka serikali iliyo Bujumbura kuchukua hatua mahsusi zenye lengo la kurejea kwenye utawala wa kikatiba ikiwemo (a) kurejesha mara moja Bunge ambalo ni taasisi ya kidemokrasia ambayo kwa sheria imepewa madaraka na watu wa Burundi. (b) kuondoa mara moja sheria ya kufuta vyama vya siasa nchini." Rais Museveni alitoa hoja kwa wenzake iongezwe (c). Alipendekeza wapewe muda watoke. Wapewe muda maalumu wa kutekeleza hili vinginevyo wapate cha mtema kuni kingine. Huyo ni Rais Museveni. Alitaka hatua kali zaidi zichukuliwe dhidi ya Burundi. Rais Museveni amesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam lakini hamtaki kumuona kuwa ni mtu aliyesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mnachozungumza juu yake ni Uhima wa Unyankole! Lakini hii kuhukumu watu kwa makabila yao mimi nilidhani Tanzania tumeacha! Nilidhani tutahukumu watu kwa vitendo vyao na msimamo wao; sio kusema huyu ni Mhima wa Unyankole. Atafanya nini na Uhima wake, hakuhiari kuwa Mhima. Ana msimamo; vijana hawa ukikaa nao unajisikia vizuri. Mimi mzee nilikaa na vijana wale Arusha pale nikasema; naam, huu ni uongozi mpya Afrika! Sasa tusiwabugudhibugudhi hawa kwa kuwarudisha kwenye makabila. Wako wale wanaosema kwamba hata Zenawi naye ni Mtutsi. Kuna nini? Iko lugha kwamba sasa Museveni, Kagame na Zenawi lengo lao ni kujenga himaya ya Wahima! Nani anahubiri ujinga huu? kuvuruga mwelekeo wa umoja wa nchi zetu. Sahau hilo; ni sehemu moja ya vuruguvurugu tu. Hata vita vya Bujumbura pale msifikiri ni vya ukabila tu, sivyo, kuna vurugu nyingi tu, lakini sina nia ya kulizungumza. Kwa kweli amini, viongozi hawa wameungana katika jambo hili.

**Mheshimiwa Mabere Marando, Mbunge** *anasema FRODEBU walishinda uchaguzi wa 1993, kwa nini msishawishi nguvu za wanademokrasia zilizoshinda zisaidiwe kurudi madarakani?*

**Mwalimu:** Hivyo ndivyo tunavyofanya. Mazungumzo yangu ya Mwanza yalianza na vyama viwili vile: FRODEBU, chama kilichoshinda, na UPRONA kilichoshindwa. Ilikuwa imetokea madanganyo tu, watu wanadanganywa wanadhani kwamba FRODEBU iko madarakani kwa sababu walikuwa na Rais Ntibantunganya yuko pale wakadhani ndiyo madaraka. Baada ya kwenda pale Desemba 1995, nilianza kuwaeleza wakubwa kwamba jamani nimekwenda pale, watu wanazungumza kulikuwa na jaribio la kuangusha serikali lililoshindwa. Hakukuwa na jaribio lililoshindwa la kuangusha serikali. Kwamba kulikuwa na jaribio la kuangusha serikali lililoshindwa na matokeo yake ni hii serikali ya mapatano ambayo imerudisha uhalali wa kikatiba sio kweli. Kuangusha serikali kulifanikiwa na madaraka yamerudi kule ambako yamekuwa daima; katika mikono ya UPRONA ikiungwa mkono na jeshi – ndivyo ilivyokuwa. Hayo ndiyo niliyosema Umoja wa Mataifa, Januari mwaka huu (1996). Walichofanya ni kwamba wamebakiza Rais Ntibantunganya na Bunge. Ntibatunganya hana uwezo, hafai kama Rais, lakini anafaa kama kiini macho, kificho, kwa kudhani lile jaribio la kupindua serikali halikufaulu. Kwa Watutsi wenye akili kuwapo kwa Ntibantunganya ni msaada mzuri sana. Nilipozungumza nao katika kikao kimoja cha Mwanza mmoja aliniambia: Mwalimu wanasema hawa hawana uwezo, nani anasema hawana uwezo? Sisi tuna jeshi wao wana Rais, wanataka nini zaidi? Kwa hiyo wanaye Rais, hana uwezo. Hawa hawana Rais, lakini wana uwezo na wana jeshi. Hiyo ndiyo hali iliyokuwapo pale.

Lakini ikawa wale Watutsi wa siasa kali nje na ndani ya nchi, hata kile kiini macho hawakipendi, kwa hiyo kwa kipindi chote hicho wanashinikiza hata hivyo ili Ntibantunganya atoke. Hiyo ya Rais hata kama hana uwezo hawaipendi lazima atoke kwa sababu anaitwa Rais. Burundi inaweza kuwa na Rais Mhutu? Hatima yake wamefaulu, lakini jitihada yangu ya mwanzo pale ilikuwa ni labda tunaweza kutokana na mazungumzo bado tukarudisha mapatano ya FRODEBBU na UPRONA lakini ikafanana

na yale mapatano aliyoifanya Marehemu Ndadaye. Kwa sababu alipokwisha kushinda hakuunda Serikali ya FRODEBU peke yake, asilimia 40 ya viti vya uwaziri aliwapa UPRONA, kile chama kilichoshindwa. Kwa hiyo nia yangu mimi ilikuwa kuwaeleza, tazama sasa ingawa mnashirikiana, ushirika wenu huu ni wa hovyo ambapo chama kilichoshindwa ndicho chenye madaraka na kilichoshinda hakina madaraka. Kwa nini tusirudi kwenye katiba, madaraka yarudi kwenye chama kilichoshinda kiweze kukaribisha wale walioshindwa lakini kwa misingi ya katiba. Hiyo ndiyo jitihada tuliyokuwa tunafanya kwa nia nzuri kabisa lakini UPRONA wakapinga. UPRONA walichotaka, mazungumzo yawe ni mazungumzo ya kutaka UPRONA kuimaliza FRODEBU.

Ndugu Marando anaposema tuwasaidie wanademokrasia, nafikiri ndivyo tunavyofanya; kwamba tuwafikishe hawa wakubwa mahali ambapo wanademokrasia wanaweza kurejea. Sasa kama kusaidia wanademokrasia kama mwingine alivyosema ni tuwaite tuwagawie silaha, hilo nisiulizwe mimi, mimi ni msuluhishi kama Ndugu Marando anavyosema. Kwenye swali lake lingine anasema; mimi ni msuluhishi lakini amesikia kwenye BBC nikisema kwamba wapigwe hao wapigwe hao! Sijui ni lini na wapi nilisema wapigwe hao; sistahili kusema hivyo na siwezi kusema waiteni wapigania Uhuru waje tuwape silaha.

Nadhani nilijibu kwa uzito zaidi. Wapo watu wanaoamini kwamba dawa ni kuwapa silaha Wahutu, kuwapa mafunzo ya kijeshi wawapige hawa. Kwa nini mnawaachia hawa wanaleta fujo? Kama mlivyofanya Kusini mwa Afrika, mliwafundisha wakaenda kupigana. Ni kweli tuliwafundisha na tukalazimisha mazungumzo, na kila wakati ilikuwa njia ya mapambano ya silaha inayowafikisha watu wakazungumza. Wahutu wameishaanzisha mapambano ya silaha yao wenyewe, mimi nadhani ni kuwafikisha katika mazungumzo; watazungumza.

Moja tulilokuwa hatuna ambalo ni gumu kulielewa ni kwamba kulikuwa hakuna serikali Bujumbura. Kama kungekuwa hakuna serikali Afrika ya Kusini, Mandela wangezungumza na nani? Kwa hiyo wanachotaka ni serikali; tungewasaidia kama wangefika mahali wanayo serikali. Sasa hivi

hawana serikali nikawaambia nataka niwasaidie tuzungumze tufike mahali mkawa na serikali nzuri UPRONA-FRODEBU, FRODEBU-UPRONA nzuri, yenye nguvu, iliyojengwa katika msingi wa katiba ambayo inakubalikakubalika kidogo nchini na nje ya nchi na mkifika hapo mnaamua la kufanya. Mtaamua wenyewe mnataka kufanya nini na akina Nyangoma wa CNDD. Mkisema mnataka kuwapiga kivita sasa mkatafute Jenerali mmoja awasaidie; mimi nitatoka. Mkisema mnataka kuzungumza naye basi mimi niko tayari kuwasaidieni kuzungumza. Lakini kwanza muwe na serikali. Sasa pamoja na ubovu wote uliotokea, sasa ipo serikali pamoja na kwamba hamuipendi, sio vurugu ile.

Tunachoiambia serikali, hatuipendi, tunaiambia zungumza na wanademokrasia na sababu moja ya vikwazo ni kusema zungumzeni. Ndivyo tulivyofanya na Afrika ya Kusini tuliweka vikwazo tukaendelea, tukaendelea, mpaka akatokea De Klerk. De Klerk asingetokea bila vikwazo. Vikwazo vilikuwa nyenzo – kitu kilichofanya De Klerk akatokea akaweza kuwaambia Makaburu wale vichwa maji zaidi kwamba kama hamkuzungumza na Mandela, tuna njia gani nyingine? Uchumi unakwenda. Wakazungumza. Na baadhi yetu tulisema vikwazo visiondoke vikae palepale mpaka saa ya mwisho. Mpaka tuna hakika kabisa kazi yake imekamilika. Na hivi sasa ndivyo tunavyosisitiza. Hiyo ndiyo jitihada; ni njia ya kuwarudisha kwenye njia ya demokrasia.

Lakini wapo wengine wanaofikiri kwamba njia nzuri zaidi ya kuwarudisha kwenye njia ya kidemokrasia ni kuwasaidia wapigane. Mimi nitawaambia kwa nini nadhani si vizuri; nadhani haitakuwa busara. Kama pana budi basi watapigana. Rwanda inaeleweka vibaya kwani watu wanafikiri tuna wakimbizi sasa kutoka Rwanda kwa sababu ya Serikali ya Rwanda hii tuliyonayo sasa. SIYO. Hii siyo serikali iliyofanya tuwe na wakimbizi. Serikali iliyofanya tuwe na wakimbizi iko Zaire, na jeshi lake na wauaji wengine wale wako Zaire. Tanzania tulijaribu kuwasaidia wazungumze kama tunavyojaribu kuwasaidia hawa wengine wazungumze, wakazungumza Arusha pale wakafikia maafikiano pamoja na maafikiano ya kuunda jeshi upya. Na RPF ya Rwanda walikubali kuingiza wanajeshi wao wachache ndani ya jeshi ambalo sasa liko Zaire, kikundi kidogo cha

wachache – maelewano mazuri tu pale. Kimsingi jeshi lile lililoko Zaire. Nani waliokataa? Walitia sahihi mkataba, wakashindwa kuutekeleza. Baadaye ndipo Wahutu wenye siasa kali wa Rwanda ambao walikuwa hawataki mgawano wowote wa madaraka na Watutsi wakaamua kwamba 'Hitler' atoke wakammaliza wakatafuta jibu la mwisho la 'Hitler'. Jibu la mwisho la Wayahudi ni kuwafuta wote, na hawa jibu la mwisho la Watutsi ni kuwafuta wote wafe wamalizike. Sasa wale wameua watu wengi sana wengine wanafikiria ni watu milioni nzima.

Sasa ndiyo taabu ya wasuluhishi, katika hali kama hiyo msuluhishi unakuwa huna upande, huna upande kuhusu nini, kuhusu wauaji na kafara au katika jambo gani? Katika jitihada ya namna hii katika kupatanisha watu ukweli ni nyenzo ya kusaidia, uongo hauwezi kusaidia. Huwezi kuwasaidia watu kwa kuwadanganya, unawasaidia kwa kuwafanya wakabiliane na ukweli. Kama upande mmoja unaua na upande mwingine unauawa na wewe unasema wewe huna upande, huu ni upuuzi. Nilisema hivyo 1994. Halafu watu wakasema Mwalimu Mtutsi. Mimi si Mtutsi mimi ni Mzanaki. Hili siyo suala la Uhutu na Ututsi, hili ni suala la haki na uovu. Wenye siasa kali wa Rwanda waliokuwa hawataki kugawana madaraka eneo lolote lile hata lililofikiwa kwa majadiliano Arusha walikuwa ni Wahutu. Wenye siasa kali wa Burundi ambao hawataki kugawana madaraka ya namna yoyote ile hata ile waliyofikia wenyewe katika majadiliano katika kitu kinachoitwa Serikali ya Mapatano ni Watutsi. Kwa hiyo huwezi kuhukumu watu hawa kwa kusema unahukumu Watutsi tu au unahukumu Wahutu tu, unahukumu vitendo vyao. Kafara wa Rwanda walikuwa Watutsi, kafara wa Burundi ni Wahutu; huwezi kupendelea Wahutu tu au unawapendelea Watutsi tu. Ukidai mimi ni Mhutu tu, Wahutu wa Rwanda wameua Watutsi wengi sana, hatuwezi kutetea Wahutu, tunatetea haki.

Mimi nilidhani Watanzania tumekomaa vya kutosha kutetea haki sio kutetea makabila. Mkianza kutetea makabila mtajipatia taabu kubwa, mtajikuta katika hali ngumu. Huyu ana panga anaua lakini mnasema huyu ni Mhutu. Hayo ndiyo matatizo ya usuluhishi; mimi tangu nilipoanza kusema hebu, hebu kuna nini hapa! Hawa tunazungumza juu

ya chama cha wengi na unafikiri chama cha wengi kiko madarakani, hapana, sivyo. Chama kilichoshindwa katika uchaguzi ndicho kilicho madarakani. Lakini nilipoanza kusema hivyo wakasema Mwalimu anapendelea. Hapana, nilikuwa nasema ukweli, huwezi ukawa unapendelea kwa kusema ukweli! Siwezi kuwasaidia Warundi kwa kuongopa juu yao au kuwafumbia macho juu ya ukweli wenyewe. Lazima kwanza tuseme ule ukweli wenyewe halafu ndipo tusaidie. Pale wanaponiambia Mwalimu unaanza kuwa mkweli kupindukia, na waseme, kweli hawafai, nitajiondoa watafute muongo awasaidie.

**Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge** *alisema, sasa Mwalimu Burundi tu, Zanzibar, je?*

**Mwalimu:** Sasa Ndugu Marmo nifanyeje? Nilipoombwa nisaidie jambo la Rwanda mwaka jana, la Rwanda lilikuwa jepesi halikuwa na matatizo sana kwa sababu ilikuwa ni jitihada za kuwasaidia wakimbizi kurudi nyumbani. La Burundi nilisema ngoja kwanza nione, nikataka tutimize masharti fulanifulani kabla sijasema kama nitaweza kusaidia ama sitaweza kusaidia. Sharti la kwanza ni kwamba wahusika hawana budi waseme Mwalimu njoo, utusaidie – wahusika wa pande zote mbili. Hili ni sharti la kwanza. Upande mmoja wanasema tu njoo utusaidie, nakwenda pale, FRODEBU wanasema njoo UPRONA hawataki au kinyume chake haina maana. Kwa hiyo, katika jitihada ya kusaidia katika usuluhishi lazima pande zote mbili zikubali. Sharti la kwanza ni hilo. Hilo niliwaambia mapema.

Sharti la pili, ni kwamba unalielewa tatizo lenyewe. Nilisema nipeni muda kwanza nilielewe tatizo lenyewe. Kwa hili nikaenda pale Desemba, nikaenda Januari, nikaenda Februari, nikaenda Machi, nadhani halafu nikaona ninaanza kulielewa vizuri tatizo la pale. Sharti la tatu, uone hata baada ya kulielewa tatizo lile, mwenyewe uamue labda ninaweza kusaidia. Maana unaweza kulielewa ukaona hili simo baada ya kulielewa ukaona hapana hili siliwezi hata kidogo. Ulielewe halafu usema labda naweza kuwasaidia hawa. Lazima niyatimize masharti yote matatu haya. Nikayatimiza, nikakubali baada ya miezi mingi.

Sasa Ndugu Marmo masharti hayo…! *(Mwalimu aliachia hapo, hakuendelea kujibu swali hilo).*

**Mheshimiwa Pius Ngeze, Mbunge** *yeye alisema anaunga mkono juhudi hizi lakini akataka kujua kwamba wapo wenye mashaka juu ya vikwazo. Nani wenye mashaka? Akataja Wafaransa na Wabelgiji.*

**Mwalimu:** Sasa sitaki kusema Wafaransa na Wabelgiji wana mashaka na vikwazo kwa sababu katika hili mimi ni msuluhishi. Tunachotaka ni kupanua, kuongeza idadi ya wale watakaosaidia katika kufanya vikwazo hivi vipate matokeo tunayotaka. Haiwezi kuwa kazi yetu sisi kuongeza idadi ya watu watakaopinga vikwazo hivi, kazi yetu ni kuogeza idadi ya watakaosaidia na sio kuongeza idadi ya watakaopinga. Kwa hiyo bila kuwa na hakika kuwa wanapinga, sitaki niseme kwamba wanapinga. Sina hakika kama Wafaransa wanapinga, Wabelgiji wanapinga: kwa hiyo sitaki niseme kwamba wanapinga.

Kabla ya Arusha tulifanya mkutano Dar es Salaam: mimi, Salim, (Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi za Kiafrika), jamaa mmoja anaitwa Howard Wolpe, mwakilishi wa Rais Clinton, Aldo Ajello ambaye Umoja wa Nchi za Ulaya wamemteua ashughulike na jambo hili la Burundi – Ajello alikuwa mwakilishi wa Umoja wa Mataifa katika tatizo la Mozambique; halafu tulikuwa pia na mwakilishi maalumu wa serikali ya Ubelgiji kwa shughuli hii ya Burundi, na Balozi wa Marekani, tarehe 18/7/97 ndiyo siku niliyopata mjukuu yule niliyemwita Rwagasore. Tukazungumza nao; na wote wale tunaelewana vizuri sana sana juu ya jambo la Burundi. Hiyo ilikuwa siku moja kabla ya kuangushwa serikali, siku moja kabla ya kuangushwa serikali, Umoja wa Mataifa wakapitisha azimio kali sana kwa sababu ilielekea kwamba huenda kutakuwa na kuangushwa serikali. Linakumbushwa katika taarifa ya pamoja hii, linakumbushwa lile azimio kali la Umoja wa Mataifa kwamba hatutakubali serikali inayotokana na kuangushwa serikali. Umoja wa Nchi za Ulaya vilevile walitoa tamko la namna hiyo.

Nasema tulifanya mkutano pale tukaelewana, tuna msimamo uleule na wale wanaowakilisha kwao, na mimi katika upatanishi wangu huru na wa kujitegemea kwangu tunaelewana katika msimamo huo huo wa kupinga.

Halafu kuangushwa serikali kumefanyika, halafu tukaitisha mkutano huu; kikao cha kwanza cha Kampala cha Marais wetu Mkapa na Museveni, wawili; halafu mimi kabla ya kwenda Arusha nikaonana na Buyoya pale Butiama. Nimeenda Arusha wote wapo, Howard Wolpe yupo, mjumbe wa Ulaya Ajello yupo, mjumbe wa Ubelgiji yupo na mjumbe wa Umoja wa mataifa tulikuwa naye katika mkutano wa Dar es Salaam na Rais aliwaalika katika mkutano wa Arusha. Tulifanya mkutano ule tukaumaliza na wote wakafurahia sana matokeo yale. Wote pamoja na mwakilishi wa Ubelgiji. Huyu ndiye mwakilishi wa Ubelgiji. Alikuwapo kwenye mkutano na akatupa mikono ya pongezi kwa msimamo. Mimi ni msuluhishi, hili ndilo ninalolijua, jingine sijui. Leo hii ninaonana na watu hao wote watatu, na yeye ataniambia kwamba Mwalimu nilikupa mkono wa uongo? Kabla ya hapo ni busara nisiwachokoze Wabelgiji kwa jambo ambalo sina ushahidi nalo. Nina ushahidi kinyume halafu niseme Wabelgiji wanapinga. Hilo la kwanza juu ya Wabelgiji.

Wafaransa. Jana nilikuwa na mkutano wa Mabalozi. Niliwaeleza Arusha tumeamua nini. Balozi wa Ufaransa akaniuliza Mwalimu humu mnasema mnataka jumuiya ya kimataifa isaidie hatua hizi mlizochukua, mnataka tuisaidie nini? Nikasema tunataka mtusaidie mawili; kwanza kabisa ungeni mkono uamuzi huu wa viongozi hawa. Ungeni mkono kitendo hiki na uamuzi wao. Itakuwa jambo la ajabu sana kwamba wote tutakuwa tunapinga kuangushwa serikali halafu ikatokea kwenye vitendo wenzetu mturuke. Viongozi wamekataa mambo mawili walipokutana Arusha, wamekataa kusema kwamba Buyoya ni Bwana mtu mwema kwa hiyo tumpe muda. Tulikwisha mlaani. La pili wamekataa kukutana na kuandika maneno makali makali halafu mrudi nyumbani; hawakupenda maneno mazito lakini yasiyokuwa na kitu ndani yake, wamekataa. Safari hii wameamua watende na uwezo wa kutenda wanao. Nchi zile zilizokutana pale ndizo zina uwezo wa kutenda jambo na Burundi ikasikia. Wakaamua kutenda. Sasa tunataka ninyi wakubwa mnaosema tunasaidia, tunaunga mkono, tunaomba juhudi hizi nazo muunge mkono. Kwanza kisiasa. Pili, nchi yoyote miongoni mwenu ambayo inaweza kufanya kitendo cha kuimarisha dhamira ya hawa ifanye. Swali niliulizwa na Balozi wa Ufaransa; usoni niliona kama ameelewa, sasa mimi sisomi

ndani lakini niliona ameelewa hivyo na mabalozi wengine niliona wameelewa hivyo. Baadaye nilipokwisha kufika huku nikaletewa tamko la Marekani. Balozi wa Marekani akanitumia kwa 'fax' hapa nikapata msimamo wa Marekani. Hatujaambiwa nchi yoyote inayopinga. Tunataka jambo hili lifanikiwe. Sioni kwa nini ninapoambiwa jambo hili naunga mkono, mimi niseme lakini huungi mkono, naona haitusaidii sana. Watakapojitokeza tutasema.

**Mheshimiwa Idd Simba, Mbunge** *Ombi: Baraza la Wadhamini la Nyerere Foundation nalo liwe na Waafrika wengine nje ya Tanzania.*

**Mwalimu:** Baraza ndiyo maana halijakamilika. Hawa Watanzania wamekamilika, bado tunatafuta majina mengine ya watu kutoka nje. Tuko katika jitihada ya kuwapata, bado tunafanya jitihada za kuwapata. Mama yangu pale anataka tuwe pia na Mtutsi na Mhutu kwenye Baraza. Sasa unaanza kwenda ndani mno. Lakini tutajitahidi kuwapata na wengine kutoka nje. Hatukutaka wawe wengi sana maana gharama ya kuwaita itakuwa juu sana. Tulifikiri tupate wachache kwa sababu kuna tatizo la kupata akid tukiwaita.

Ndugu Simba vilevile anasema, katika ripoti yetu ya 'Majukumu ya Nchi za Kusini' ambayo inasema "Nchi za Kusini lazima zitumie hadi upeo wa mwisho, uwezo wa ndani kwa ajili ya maendeleo". Ndugu Simba anasema sasa hapa kwetu, je, mbona hatufanyi? Sasa mnaniuliza mimi badala ya kufanya? Mmo katika uwezo mzuri sana wa kufanya. Sisi tumesema fanyeni, hamna budi kutumia rasilimali zenu za ndani, zitumieni, kujitegemea kitaifa katika maana ya nguvu kazi, na fedha – tumieni uwezo wenu hadi upeo wa juu. Mimi sifanyi zaidi ya hapo, nitakuwa nakwambia Simba unafanya nini? Hamuwezi kusema Mwalimu Nyerere anatuzuia; sasa ni ruksa!

**Mheshimiwa Fatma Magimbi, Mbunge** *aliuliza kama alivyouliza Iddi Simba juu ya kuongeza wajumbe wa Afrika katika Baraza la Wadhamini.*

**Mheshimiwa Halimeshi Mayonga, Mbunge** *aliuliza, vikwazo vya uchumi visipofaulu kwa haraka uwekwe msimamo wa kuvamia.*

**Mwalimu:** Hili nililijibu na niwaombeni msaada. Mambo haya wakati mwingine yanasemwa kama kwa mzaha. Mimi ni muumini kabisa wa umoja wa nchi za Afrika lakini si muumini wa umoja wa kuteka ama kumeza nchi. Mimi ni muumini sana sana wa umoja wa nchi za Afrika. Nchi zetu hizi mipaka tuliyoaachiwa na Mkoloni ni bugudha. Ni vizuri ikaondolewa. Lakini mimi si muumini hata kidogo wa umoja wa kuteka ama kumeza nchi. Nilisema na ninalirudia. Imani yangu ni hiyo ya kupinga umoja unaokuja bila maafikiano mazuri. Mnakaa wote mnaelewana kwamba hili jambo la kukaa peke yetu peke yetu, mbali mbali, halifai. Wote mnakubaliana, mnaungana. Niliwaelezeni, ndiyo ilikuwa chanzo cha Katiba ya Muungano wa Tanzania. Sipendi nchi moja ya Afrika ijaribu kumeza nchi nyingine. Ninazungumza habari ya umoja wa kukaa mkaona wote matatizo, baada ya kuona matatizo yale mnasema kwa nini tunakaa kwa mbalimbali, tuungane, tuyatatue kwa pamoja. Umoja ninaozungumza mimi ni umoja huo wa kukutana. Wabunge mtatusaidia. Kwa kweli ndiyo njia peke yake. Mbunge haifai kusema jambo kwa utani. Kila mnalolisema linachukuliwa kwa uzito na umakini mkubwa.

Mimi nazunguza habari za Umoja. Niliwahi kusimama Dar es Salaam pale na kusema: vyema mimi sasa hivi najitahidi kusaidia Warundi hawa kupata usuluhishi. Mungu akisaidia tutaupata watakuwa na Serikali nzuri pale. Lakini utatuzi huu ni kama 'aspro' kwa matatizo haya. Katika nchi ndogo ndogo hizi kama Burundi na Rwanda ambapo wamebanana, pale katika ardhi ile, ukiuliza nani kanibana wanasema Mhutu au Mtutsi kanibana. Kama ingekuwa wako katika eneo kubwa zaidi hivi, badala ya kaeneo kao kadogo, watasema nani kanibana, nani, nani kanibana? Maana nchi kubwa hii, wala usingesikia, kama Afrika ingekuwa imebaki kama ilivyokuwa. Wangetoka, wangeingia Ngara na msingewaita wakimbizi maana ni kwao. Sasa mnawaita wakimbizi kwa ajili ya mpaka, ni wenzetu wale, mkiweka vikwazo mnaua ndugu zangu. Tuna mpaka pale, Warundi na Wanyarwanda ikitokea shida pale wanakuwa kama wanyama wa Serengeti, wale katika hali ya shida hawautambui ule mpaka wanavuka

tu, hawajali na hawaogopi. Hawautambui mpaka ule. Nchi hizi mzisaidie, kama zingekuwa ni maeneo makubwa wala msingekuwa mnasikia habari za Wahutu na Watutsi, kama ingekuwa ni sehemu au eneo la nchi kubwa.

Hapa niliwahi, katika shughuli zangu za kazi huko Kilimanjaro; kila nikienda Wachaga waliniambia Mwalimu ardhi hakuna. Niliwaambia, tazameni mimi sina uwezo wa kupanua mlima Kilimanjaro, lakini Tanzania ni kubwa. Ndipo tukaanza kuwapeleka Wachaga wale Mpanda na wengine Morogoro; hivi leo wamezagaa pote! Kama mngewaacha pale na ka-mlima kale wakaachwa peke yao eti nayo ni nchi, hivi leo mgesikia kwamba Wachaga wa wapi si Wachaga, Wamarangu si Wachaga, wangechinjana. Hali kadhalika na kote ambako watu wamebanana. Tanzania ni kubwa, Tanzania ni yao. Mpaka leo bado nasema hivyo. Warundi, Wanyarwanda nakaa nao nasema hivyo hivyo.

Halafu anatokea Mbunge anasema sasa Mwalimu dawa ni kupeleka jeshi tu, kaBurundi kachukuliwe na Tanzania, na kaRwanda kachukuliwe na Uganda, tatizo linakwisha. Hii lugha ya Mbunge wa wapi? Utani au umakini? Kwa sababu kama wewe Mbunge hujichukulii kwa umakini na uzito, je, wenzako nje wanakuchukulia kwa umakini na uzito kwa sababu ni Mbunge na hawatazamii Mbunge kusema kihuni. Ikiwa lugha ni kuteka ama kumeza sio umoja wa kukaa mkazungumza ni umoja wa kuteka ama kumeza, pana kazi hapa!

Nilipokuwa Umoja wa Mataifa walizungumzia kuingilia kijeshi. Nikawauliza, halafu iweje? Mnataka kuirudisha Burundi kwenye ukoloni? Unamaanisha nini unaposema kuingilia kijeshi, muwakabidhi Wabelgiji tena watwae Burundi kuwa koloni lao au muwakabidhi Wajerumani? Majibu ya baadhi ya Wabunge hapa ni: ikabidhi Tanzania! Wengine wanasema ilikuwa yetu; ilikuwa yenu wapi? Burundi haijawahi kuwa sehemu ya Tanzania hata siku moja wala Rwanda haijawahi kuwa sehemu ya Tanzania hata siku moja, na kama unafikiri iliwahi kuwa basi Tanzania ilikuwa sehemu ya Burundi, na Warundi wadai Tanzania waseme ilikuwa yetu au Wanyarwanda wadai waseme Tanzania ilikuwa yetu ile. Sasa wamekuja wako Ngara! Kwa nini mnapendelea upande mmoja? Sasa Wanyarwanda wamekuja wamechukua nchi yao wako Ngara pale, sasa

kuna shida gani? Acha kuzungumza lugha ya ubeberu katika Bunge la Watanzania!

**Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge** *naye alizungumzia jeshi la kimataifa.*

**Mwalimu:** Labda nimelijibu kwa sababu Warundi nakaa nao nasema, iwapo mnafikiria kwamba lipo suluhisho la kijeshi la tatizo lao, mimi simo. Mimi siwezi, kuwasaidieni, na ninyi kama mnafikiri lipo suluhisho la kijeshi nitaacha kuwa msuluhishi. Nitasuluhisha nini? Ila nimesema kama fujo zinaendelea na kina Buyoya hawa wanafikiri dawa ni kuwapiga Wahutu na halafu inaanza matatizo kama ya Rwanda, hatuwezi kukaa tu na kuona Rwanda nyingine inajirudia Burundi. Lazima tuingie bila idhini, bila kuomba idhini yoyote. Kama ni jambo la kuzuia tu mauaji tungeweza kufanya Rwanda. Tungeweza kuingia, tungepunguza sana mauaji. Ninachosema sasa hivi tusikae kimya, kama yanatokea matatizo kama yaliyotokea Rwanda mimi nasema ingia. Lakini hilo ni kuzuia mauaji sio kutatua tatizo. Tatizo linabaki palepale.

**Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge** *yeye ana usemi wake wa Kiingereza mimi sijawahi kuusikia – 'If you want to cure you must wound' (Ukitaka kutibu lazima ujeruhi).*

**Mwalimu:** Unakuja unanikuta sina jeraha lakini una haja sana ya kunitibu basi unanijeruhi kusudi. Lakini, sivyo alivyokuwa anakusudia kusema; anasema; je, vikwazo tusipofanikiwa, tufanye nini? Vikwazo mimi nadhani tutafanikiwa maana tunafanya kitendo kiwapeni matokeo mnayoyataka. Kulikuwa na vikwazo vya Rhodesia tukadhani havitafanikiwa lakini vikafanikiwa. Ilikuwa vikwazo viliunganishwa na mapambano ya silaha. Vikwazo vya Afrika ya Kusini hivyo hivyo viliunganishwa na mapambano ya silaha. Kuna watu walisema vikwazo haviwezi, uongo, viliweza. Wala msifikiri kwamba vikwazo vya Afrika ya Kusini vilichukua muda mrefu sana kabla ya kuondoa Siasa ya Ubaguzi wa rangi. Vikwazo vya Afrika ya Kusini havikufanya kazi! Si kweli! Vilifanya kazi; ndivyo vilivyomzaa De Klerk; bila vikwazo msingemsikia De Klerk hata kidogo. Tena pale ni vikwazo zaidi kuliko mapambano ya silaha. Wangeendelea Makaburu na jeuri yao ile ile. Lakini pale vilifanya kazi vikwazo zaidi kuliko mapambano ya silaha.

Hapa sitaki kuwaambieni kwamba hii italeta matokeo yaleyale. Lakini 1972 wakimbizi wetu wa Burundi ni wa siku nyingi. 1972 tulipata wimbi kubwa sana la wakimbizi wakati wa Micombero, wengi. Nikampelekea ujumbe Micombero – acha kuua watu, wewe hukuwa Rais wa kuua watu. Nikamwambia, acha, akafikiri tunamtania. Acha, akaendelea. Tukamwekea vikwazo bila kumtangazia mtu. Bila kumtangazia mtu tulifunga bandari ya Dar es Salaam; tulifunga kimyakimya tu. Alikuja katika muda wa wiki moja. Hatukutangaza, tulinyamaza kimya, tukanong'ona tu na vijana kwamba vitu vya Burundi hakuna kupita hapa. Katika muda wa wiki moja akaja Mwanza akapunguza punguza fujo zake. Wala hatukuzungumza na Kenya, ilikuwa Dar es Salaam tu. Sasa hii wameamua watu wakubwa hawa, hizi nchi kubwa zimeamua zote. Sasa simtegemei Buyoya katika muda wa wiki moja lakini nina hakika vikwazo vitafanya kazi. Bora isivurugwe tu na wakubwa. Tunawaambia wakubwa hawa kwamba kama ninyi hamwezi kusaidia sasa tunachowaomba ni kwamba msivuruge tu. Dhamira ya viongozi hawa kufunga ni kubwa.

Jana nilipata habari Buyoya anasema tuliambiwa kwamba itachukua wiki mbili ndipo vikwazo vianze lakini sasa mbona vimeanza. Kwa sababu malori tayari yanarudishwa mpakani pale. (Kwa Waziri Mkuu Sumaye) Uzuri wa serikali yako inafanya kazi haraka sana. Mimi naamini kwamba, iwapo havitafanya kazi na iwapo tumedhamiria kuondoa ubaguzi wa rangi uliobaki hatuwezi kuachia pale hauna budi kuondolewa sasa. Kama tunataka kutokuwa na wakimbizi zaidi lazima tuingie mpaka chanzo na kiini chake kimalizike pale. Hasa Watanzania lazima kuwa 'completely open minded' katika kufikiria haya. Najua Watanzania mmeanza kuchoka. Mambo makubwa hayafanywi na watu wasiokuwa na subira.

**Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi, Mbunge** *anasema umoja wa Afrika ni kama kidonda ndugu, hautokei.*

**Mwalimu:** Tunazungumza, kuchelewa hakufanyi kwamba liwe halina maana. Lazima tukusudie kweli. Ulaya pale walianza mwaka 1957. Nchi chache tu na watu wachache, kwa kweli walikuwa watu fulani fulani tu mmoja alikuwa kiongozi, Monnet, wa Ufaransa. Pale walisema kwamba lazima waanze hatua ya kuwashirikisha wazungu; bila

kuwashirikisha wataendelea na vita vyao hivi. Wakaanza na sehemu ndogo sana tangu 1957. Wanakwenda, nchi zinapanuka; nchi shiriki zinaongezeka lakini hata umoja wenyewe unajiimarisha zaidi kule Ulaya, inaendelea hivyo hivyo. Lakini wakina Monnet walishakufa lakini jitihada zinaendelea. Hatima yake nchi zile zitaunganika mwishoni.

Ni kweli tunazungumza kama donda ndugu umoja, umoja; lakini umoja hauwezi kuja kwa kuimba, lazima wapatikane washabiki na Profesa tutafurahi sana ukiwa mmoja wa washabiki wa kuleta umoja wa Afrika. Ushabiki na kutenda vitendo mbalimbali. Vitendo vitakuwa ni vya aina mbalimbali. Moja ni wasomi wanashirikiana, na wanawake wanashirikiana, wafanyakazi wanashirikiana, vijana wanashirikiana, wengine wafanyabiashara wanashirikiana. Umoja wa Ulaya umesukumwa sana sana na wafanyabiashara wa Ulaya. Wafanyabiashara wa kwanza wakubwa wakubwa wanasukama sana umoja. Kosa letu moja katika kizazi changu mimi wakati tunashughulikia Umoja wa Afrika tuliachia warasimu kusimamia umoja. Sasa tuache. Sasa warasimu tuache kusimamia umoja. Uongozi wa Serikali lazima viwemo vyama vya kiraia, sasa chama cha kiraia, watu wa kila aina, ndio wasimamie umoja – 'a movement of African Unity'. Sasa undeni; mnangojea nini? Waumini katika chama cha kiraia wafanye. Watasaidia zaidi kusukuma kwa sababu wapo wale wanaofikiri kurudi kwenye makabila, na kurudi kwenye makabila kutakuwa na marais wengi zaidi na mawaziri wakuu wengi zaidi, mawaziri wengi zaidi na maspika wengi zaidi. Chama cha kiraia lazima kiingie, lazima kuwe na 'a movement of African Unity'. PAFMECA ilikuwa vuguvugu la ukombozi wa Afrika. Sasa undeni, mnafanya nini, hakuna! Sasa undeni! Sasa tuna maprofesa lazima washughulike, washughulikie umoja wa Afrika. Msiache wazee ndio washughulikie mambo ya umoja. Profesa, sasa nataka kuandikisha watu katika Foundation, tunataka watu ambao kweli wanaweza kuwa washabiki wa Umoja waAfrika, kusaidia kuhubiri, kusimamia, kuona kuwa nini matatizo yapo, hasa kwa nini hatu-*move*, tunayapata matatizo, tunayaelewa halafu tunajaribu kuwashawishi viongozi wa nchi zetu kwamba tatizo hili likitoka hapa pengine tunaweza kupata *movement* nzuri zaidi ya umoja Tusinung'unike tu tukasema kwamba Tanzania tumesaidia kukomboa Afrika ya Kusini lakini mpaka

leo hatuoni faida yake. Mnataka mpate faida gani? Tuanze, tushirikiane maana tumeishaona faida ya Uhuru sasa tutafute na mengine. Tufanye kazi tusingoje matunda kudondoka. Matunda ya Umoja lazima yafanyiwe kazi, matunda ya Uhuru lazima yafanyiwe kazi, matunda ya ushirikiano lazima yafanyiwe kazi. Afanye nani na wengine wavune tu?

**Mheshimiwa Henry Shekifu, Mbunge** *Swali lake la kwanza linasema kwa nini South Centre iko Geneva? La pili, mitaji mikubwa ya maendeleo yetu bado tunapata kutoka nchi za kaskazini, Ulaya, sasa tutafanya nini?*

**Mwalimu:** Kwanza tumia mali zilizo nchini kwako kwa kiwango cha juu kabisa. Mtaona kwamba matatizo ya nchi yataanza kuwa katika sura ya kweli kweli. Nichukue mfano wa nyumbani. Moja ni kulipa kodi tu. Uchumi wetu si mzuri ajabu lakini ni mzuri kiasi, na wako watu wanatengeneza pesa. Tunaanza kuwa na mamilionea hapa, watu wanatengeza pesa, wengine pesa kubwa, wengine fedha kiasi lakini watu wanatengeneza pesa lakini hawalipi kodi! Matatizo yanakuja wakati wa kwenda kuomba pesa kwa wakubwa hawa. Kadiri unavyokuwa dhaifu unapowaendea, ndivyo nao wanavyokuwekea shinikizo zaidi. Hii mnajiletea kwa kutotumia rasilimali zenu. Hii ingepunguza matatizo mengine hayo kama mngekuwa mnakusanya pesa hizo za kodi. Hii ya kutotumia rasilimali za ndani inatupa matatizo sana. Sana mnakimbia kwenda Umoja wa Mataifa, mnakwenda kutafuta nini? Juzi nilikuwa Uganda rafiki zetu pale matumizi ya kawaida yao yanalipwa na pesa za Serikali – na mapato ya ndani. La kwanza kabisakabisa ni kutumia mali zilizo nchini kwa kiwango cha juu kabisa. Zile pesa mnazopata kutoka nje si kiasi kikubwa sana. Kutumia rasilimali zenu za ndani, hiyo inapunguza kidogo matatizo. Kwanza inakupa heshima kidogo unapokaa na wakubwa wale siyo ombaomba moja kwa moja. Ukienda kama ombaomba usilalamike unapotendewa kama ombaomba!

**Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge** *anataka 'Berlin Conference' yetu wenyewe ya kuondoa mipaka.*

**Mwalimu:** Vema, kwa maana ya kwamba tunao Mkutano wa Berlin yetu ambayo ni OAU. Hakuna sababu ya kuwazuia kujadili. Mipaka hii inatusidia nini? Hii mipaka tumeirithi tu. Mimi ndiye nilitoa pendekezo

kwamba tuiheshimu mipaka ile. Imesaidia kidogo katika kupunguza magomvi baina ya nchi na nchi. Kwa kweli hakukuwa na njia isipokuwa kuiheshimu mipaka hiyo. Lakini kama viongozi wetu hawa wa sasa, hawa rafiki zangu niliokaa nao mara mbili au tatu, kama wakifikiri uwezekano wa kuweka kaMkutano kao ka Berlin, sio ka kuweka mipaka bali kuing'oang'oa mipaka hiyo, mimi nitafurahi sana. Dakta Slaa wasaidie!

**Mheshimiwa Juma Ngasongwa, Mbunge** *anauliza, je, vikwazo ni vizuri, vitafaulu?*

**Mwalimu:** Nadhani nimelijibu. Nataka watu wa ndani ya Serikali walielewe hili na ni vizuri sana kulikubali.

**Mheshimiwa Dk. Maua Daftari, Mbunge** *ananiuliza, umekata tamaa Mwalimu?*

**Mwalimu:** Sijakata tamaa. Hilo nimewambia hata Warundi ninaokaa nao wakiniudhiudhi nimewaambia kwamba kwanza msidhani kwamba mtaniudhi halafu nikaacha, siachi! Siachi kwa sababu mbili. Kwanza, mimi ninatokana na uongozi wa mwanzo ule wa Afrika. Siachi. Hivi kweli kwa sababu ya mipaka ile basi Warundi sio wenzetu, tuwaache. Siwezi hata kidogo. Wao wako Ngara pale. Wao hawaitambui mipaka ile, wana shida, lazima tuwasaidie. Siwezi kuwatia moyo kwamba waachieni, hilo siwezi kabisa. Kwa hiyo, sikati tamaa, nitaendelea na tutapata jibu la kudumu. Pili, nimewaambieni kwamba Rwagasore alikuwa rafiki yangu sana. Niliwaambia hawa viongozi wa UPRONA waliokuwa wananifanyia fujofujo. Niliwaambia angelifufuka Rwagasore angeliwashangaeni sana ninyi kukuta Chama alichoacha sasa ni cha ovyoovyo. Hakuacha chama cha Watutsi, aliacha Chama cha Warundi. Hakuacha jeshi la Watutsi aliacha jeshi la Warundi. Sasa namkummbuka mimi alikuwa rafiki yangu. Nayo ni sababu ya kunifanya nisikate tamaa, maana tunaweza kuwaheshimu hata waliokufa kwa kufanya kazi ambazo wangeweza kufanya kama wangekuwapo.

**Mheshimiwa Dk. Alex Khalid, Mbunge** *anazungumza juu ya ubabe wa Buyoya, kwamba Buyoya ananivunjia heshima.*

**Mwalimu:** Upuuzi! Mimi siwezi kusema ananivunjia heshima. Buyoya hakunivunjia heshima. Buyoya anatimiza wajibu wake. Buyoya anasema kaitwa: akaniambia, Mwalimu, mimi nilikubali sio kwa sababu ya tamaa binafsi, sina. Viongozi wa jeshi waliponijia na kuniomba nijitolee nilikubali kwa sababu nchi ilikuwa inaonekana ni vurugu, hivi, mambo yalikuwa yanaelekea kwenye vurugu. Nikakubali lakini nikawaambia kwamba mimi sina tamaa binafsi. Kama mnaweza mkapata mwingine ndani ya jeshi afanye shughuli hii mwambieni, sio lazima niwe mimi. Wakasema hapana ni wewe tu. Lakini wanaosema ni wewe tu ni nani, mmegawanyika, ni idadi ya walio wengi au ni jeshi zima. Wakasema ni jeshi zima. Ndipo nikakubali.

Buyoya akasema naomba unisadie kuiponya nchi yangu inayoelekea kwenye vurugu. Nikasema vizuri. Akasema, Mwalimu naomba ulielewe unisaidie na viongozi wa Afrika ya Mashariki walielewe wanisaidie. Nikamwambia, mimi sidhani kwamba tunaweza kukusaidia. Wewe unasema hivi, lakini wale waliokuita je? Mimi sasa Burundi, nalielewa vizuri kidogo tatizo hili. Wale waliokuita hawawezi nao kusema kwamba hawana tamaa maana tunawajua. Wengine ndio hao tangu mwanzo wanashinikiza kwamba Ntibantunganya atoke. Walikuwa hawataki hata kuiona sura yake. Wewe unasema hivyo lakini waliokuleta wanaweza wasiseme hivyo. Hatuwezi kukusaidia sisi. Hatuwezi kusaidia kwa kuwafanyia wema. Huyu kama ana rafiki zake wanaotaka kumsaidia, basi wamsaidie kama tulivyomsaidia De Klerk. Kazeni vikwazo. Kama kweli anataka kusaidiwa atakaa nao wale, atasema jamani tuzungumze, maana bila mazungumzo twafa! Sasa, kaniaibisha nini? Mimi sikuwa Rais wa Burundi. Mimi nawasaidia tu na siachi, naendelea. Ama kusuluhisha kama wanadhani bado naweza kusuluhisha, ama kuendelea kushawishi Jamii ya Kimataifa kwa kuwaambia sasa tusiliachie tena tatizo la Burundi likabaki hapohapo mpaka tulipatie utatuzi. Kama *Barundi* wataendelea kunitaka niwasaidie nikiwa msuluhishi nitafanya. Kama wakisema wanataka msuluhishi mwingine nitasema vizuri sana. Nitamsaidia msuluhishi huyo kwa kupitapita kushawishi asaidiwe huyo

msuluhishi mwingine. Namna moja ya kumsaidia ni kushughulika na Watutsi wale ili kuwasaidia Warundi kupata amani katika nchi yao.

**Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu, Mbunge** *alitaka kujua kama Foundation kazi zake zinaweza kuwa za kutatanisha na za OAU.*

**Mwalimu:** Haiwezi kuwa. Sisi, moja ya shughuli zetu tunaweza tukasaidia. OAU ni kikao cha Serikali, kama Serikali zitataka kuleta umoja wa Afrika. Kama nilivyowambia shughuli hizi za umoja wa Afrika, umoja wa Afrika hautakuja bila kukampeni, bila washabiki kufanya kazi, bila washabiki wa kuzisaidia Serikali hizo katika mambo hayo makubwa ambayo tunaamini yanastahili kufanywa. Tunataka sisi wengine raia tu tuwasaidie. Kwa hiyo, haka kachombo kamoja kadogo tu kaingie katika jitihada hiyo ya kuwasaidia viongozi. Lazima tuwasaidie viongozi tusiwaachie kazi hii. Kachombo haka si ka Serikali ni asasi isiyokuwa ya kiserikali, ni kadogo lakini kaweze kusaidia katika kusukumasukuma viongozi wetu.

**Mheshimiwa Teddy Magayane, Mbunge** *alisema vikwazo vitaua ndugu zao.*

**Mwalimu:** Jana nilikuwa na Mabalozi, na mmoja alisema hivyo hivyo kwamba Mwalimu vikwazo hivi vitaua maskini. Mimi nikawaambia, lakini maskini wanakufa hata bila vikwazo! Ijumaa ile kabla ya uchaguzi ilikuwa Rais aende kwenye mazishi ya Watutsi kama mia tatu waliokuwa wameuawa; hawakuuwawa na vikwazo. Na kabla ya hapo kulikuwa na mauaji mengine. Hawa walioua walikuwa wanalipiza kisasi cha mauaji yaliyokuwa yamefanyika vilevile hayakutokea kwa sababu ya vikwazo. Vikwazo ni shinikizo kwa wale ambao tunadhani msimamo wao ndio unaleta matatizo yote haya na mimi nadhani wataumia zaidi. Jana najua ndugu zako wale wasingeweza kuniletea ujumbe kwamba Mwalimu mbona mnarudisha magari yetu mpakani pale? Walionieletea ni hao walioleta habari, watakaoumia ni hao. Dada zako wataumia kweli lakini hawataumia kama hao wanaoendeleza vita vya wenyewe kwa wenyewe pale. Kwa hiyo tujitahidi. Ni kweli wanaumia lakini ni kuumia unapotafuta dawa!

**Mheshimiwa Hassan Diria, Mbunge** *anasema Foundation iwe jukwaa la kuzungumzia Umoja wa Afrika.*

**Mwalimu:** Si jukwaa la Afrika ni mchango wa mazungumzo. Si jukwaa kwamba sasa tunaunda jukwaa la Afrika la kuzungumza umoja, hata kidogo. Lakini ni kamchango kuwezesha watu fulani; wanakaa wanazungumza, 'kulikoni', tunataka Umoja katika Afrika, tunataka maendeleo katika Afrika, tunataka Amani katika Afrika, 'tatizo ni nini?', mbona hatufiki huko? Matumaini yangu ni kwamba kaFoundation kale katatoa mchango katika mjadala huo.

**Mheshimiwa Hassan Diria, Mbunge** *anasema katika kazi za kusuluhisha hatuna nyenzo kama za wakubwa.*

**Mwalimu:** Wakubwa, kwa mfano kule Bosnia, Marikani walipowaita wazungumuze, Marikani wanazo nyezo. Walisema kama hamkubali mtakiona cha mtema kuni. Nyenzo moja wapo ni ya silaha na nyenzo moja ni ya vikwazo. Waliamini wakubwa hawa kwamba Serbia iliyobaki, kwamba wao ndio wanaoleta fujo; kwamba wao ndio waanzilishi wa fujo. Kwamba wao bila kushirikiana hatuwezi kupata amani kule. Waliwawekea vikwazo. Serbia wamewekewa vikwazo na walipoitwa kwenye mazungumzo Rais wa Serbia alibanwa. Marikani walisema lazima ushiriki au la vikwazo vinaendelea. Tunajua wewe unaweza kusaidia kuleta utatuzi. Vikwazo vipo. Hivi sasa kuna watu wawili wanatafutwa, ambao wanadhaniwa wameshiriki katika mauaji, wapelekwe 'The Hague' kwenye mashitaka. Hata hilo wanamwambia kama hukuwaleta, vikwazo vinaendelea. Nani anasema vikwazo havifanyi kazi? Wangejuwa wakubwa hawa kwamba vikwazo havifanyi kazi wangevitumia wao pale? Vikwazo vinafanya kazi vikiamuliwa kutumiwa. Kwa kweli, unatakiwa uwe na nyenzo hiyo, ukiwa na nyenzo hiyo, inawezekana. Lakini nasema wanazo hawa viongozi wetu waliokutana Arusha. Uwezo wanao, na nadhani na nia wanayo, na sababu wanayo! Hawakuamua kufanya jambo ambalo hawana uwezo nalo, wameamua kufanya jambo ambalo wana uwezo nalo. Na nadhani wana uwezo nalo kuliko nchi nyingine yoyote duniani. Hawa ndio wenye uwezo mkubwa zaidi katika hili.

**Mheshimiwa Eliakim Simpasa, Mbunge** *anasema aliniona wakati niking'atuka. Anasema: Mwalimu ungejua kwamba utapata matatizo hayo ungekubali kung'atuka?*

**Mwalimu:** Sasa nayajua, unataka nirudie u-Rais? Nafanya, nafanya kazi; ni kazi tu, ni shughuli za wajibu, nazifanya. Napenda sana kukaa Butiama ni pazuri kweli lakini ufanyeje. Sasa nifanye nini, nafanya hizi kazi.

**Mheshimiwa Eliakim Simpasa, Mbunge** *anauliza: Jitihada zako za Burundi zimefanikiwa kiasi gani?*

**Mwalimu:** Vema, zimefanikiwa. Kusema kweli haijawa kupoteza muda. Sio kweli kwamba muda umepotezwa. Yameleta uwazi, suala sasa liko wazi. Pengine kwa kweli tusingehangaikahangaika hivi. Kuna uwazi sasa na tunaweza kufikiri kwa makini jinsi ya kulikabili tatizo. Kwa sababu kulikuwa na mkanganyiko mkubwa. Nadhani moja ambalo tumefaulu ni kupunguza mkanganyiko na kufanya uwazi kidogo, masuala ni yapi, na kuzitafutia ufumbuzi. Nadhani wakati ule haukupotea.

**Mheshimiwa Eliakim Simpasa, Mbunge** *anadhani dawa ni jeshi liende na limng'oe Buyoya na kumrudisha Ntibantunganya*

**Mwalimu:** Hili nalo nilieleze kidogo. Ukimng'oa Buyoya umrudishe Ntibantunganya, mtaona katika hii taarifa ya pamoja, ile sura ya 7 niliyowasomea. Kwa sababu tunajua tatizo, tunajua tatizo la pale na hali ya pale tunaijua. Sura ya 7 hii ina (a) "Kurudisha mara moja Bunge ambalo ndilo taasisi halali kisheria na itokanayo na sauti ya Warundi. Kile ni chombo, taasisi halali kisheria na itokanayo na sauti ya Warundi." Kile ni chombo cha kidemokrasi, uhalali wake hauna mashaka hata kidogo. Kurudisha mara moja Bunge ambalo ndilo taasisi halali kisheria na itokanayo na sauti ya Warundi. Kurudishwa mara moja vyama vya siasa ambavyo vilisajiliwa kwa misingi ya sheria chini ya katiba, ni halali kisheria kabisa. Unaona hakuna (c) kumrudisha Ntibantunganya. Hakuna, kwa sababu ile serikali ya mapatano haikuwa halali kisheria. Ile serikali waliyoweka pale haikuwa halali kisheria kiko hiki kisingizio hiki kwamba kulikuwa na serikali halali pale ; kwamba kulikuwa na serikali halali kisheria ambayo imeondolewa na Buyoya. Ni batili moja imeondoa batili nyingine.

Tunachoshinikiza sisi ni kurudi kwenye katiba. Sio kurudi kwenye utovu wa uhalali mwingine tena wa kutuletea mkanganyiko uleule tuliyokuwa nao ambao hauna maana. Kusema kweli wengine wanasema hata hii si inaleta mkanganyiko tu. Mtu amepindua serikali halafu mnasema arudishe Rais wa zamani. Kwa kweli akimrudisha itarudisha mkanganyiko uleule kwamba hapa kuna kitu halali kisheria. Kwa nini msiache hivi hivi tu batili hii halafu mpambane na batili hivi hivi ilivyo uchi. Halafu tutafute jibu. Hata kama mnaliingiza jeshi pale – ambalo sipendekezi hata katika ndoto zangu! Lakini sio limuondoe huyu na kumrudisha Ntibantunganya. Hapana. Huondoi utovu wa uhalali wa aina moja na kurudisha wa aina nyingine Jitihada hapa ni kurudi kwenye uhalali wa kisheria chini ya katiba. Au kurudi kwenye serikali, serikali inayotokana na makubaliano hata ile ile serikali nyingine lakini inayokubaliwa na chama kile kilichoshinda na wengine wale na halafu wanaweza kuamua jinsi ya kurudi kwenye uhalali sio hii ya mtutu wa bunduki.

**Mheshimiwa Mary Nagu, Mbunge** *aliuliza juu ya suala la ubaguzi katika nchi za Burundi na Rwanda.*

**Mwalimu:** Nadhani ile ilikuwa ni kauli tu kwamba nje ya Burundi na Rwanda hawa ni Banyarwanda na Barundi. Haswa, ndiyo maana yangu. Kama wangekuwa katika sehemu kubwa wangesema sisi Barundi au sisi ni Banyarwanda. Sisi Barundi tunasema hivi, sisi Banyarwanda tunasema hivi kwa kulingana na Watanzania, kwa kulingana na Wakenya na kwa kulingana na Waganda. Unapowaacha peke yao wanafikiri kwa misingi ya Watutsi, Wahutu.

**Mheshimiwa Mary Nagu, Mbunge** *anauliza: umoja wetu umesogea baada ya Afrika ya Kusini kuwa huru?*

**Mwalimu:** Walau sasa tunaweza tukaujengea mazingira bora. Huwezi kukaa chini na Makaburu mkazungumza habari za Umoja. Walau sasa tunaweza kukaa na Mandela na kuzungumza Umoja.

Nilisema tangu awali kwamba sitakuwa na nidhamu kama ya kwenu lakini nimejitahidi, nimefika mwisho.

# SEHEMU YA TATU

## Waziri Mkuu

**Mheshimiwa Frederick Sumaye:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri mtakubaliana na mimi kwamba Jumamosi yetu imetumika vizuri.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wageni mnaotusikiliza, Maaskofu, Waheshimiwa wote ambao mmekuja kumsikiliza Mwalimu. Mimi kwa niaba yenu napenda nimshukuru sana kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. Kwa kweli Mwalimu amefanya kazi nyingi, haikuwa kuja kuzindua Foundation peke yake, na kueleza mambo ya Burundi. Nadhani mtakubaliana na mimi kwamba ametuelimisha kuhusu mambo mengi. Ameanza kutufundisha juu ya South Commission mpaka kwenye South Centre. Mambo ambayo nina hakika si wengi hawakuwa wanayaelewa kama ambavyo sasa tunayaelewa. Mwalimu tunashukuru sana. Shukurani za kumshukuru mtu kama Mwalimu ni vigumu sana kuzimaliza, na mara nyingi ni vizuri kumshukuru kwa uchache kwa sababu ukimshukuru kwa mengi hutamaliza na bado utajisikia hujasema yale uliyotaka kusema. Nimshukuru Mwalimu kwa mambo yote ambayo ameifanyia nchi hii; sote tunayajua. Tumezungumza mambo ya Burundi, sisi sote tunajivuna katika hali hii kwa sababu kubwa ya Mwalimu. Kwa hiyo, Mwalimu tunakushukuru sana kwa mambo yote ambayo umeifanyia nchi hii, na tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba uko nasi, tunapata bado nafasi ya kutumia na kutegemea busara zako. Tunakushukuru leo kwa mambo uliyotueleza. Mambo ya Burundi kama ulivyoona mwenyewe yametawala uwanja hapa. Kweli ni kazi ngumu uliyonayo, tunakutakia kila la heri. Kama tukisema tunakuonea huruma tutakuwa tunakutisha. Mimi nadhani sisi tukutakie kila la heri na tunakuahidi Bunge hili litakupa kila aina ya msaada ili uweze kufanikiwa katika jambo hili la kuhangaika na kusuluhisha wenzetu wa Burundi. Tunaamini kwamba kazi hii utaiweza. Waliokuchagua hawakukosea, na nadhani kama si wewe itakuwa kazi ngumu ambayo haiwezekani.

Nikushukuru kwa Mwalimu Nyerere Foundation ambayo leo umekuja kutueleza na kuizundia rasmi. Kama ulivyotueleza ina maeneo makuu; hasa ya kuleta Amani, Umoja na Maendeleo. Lakini maendeleo ya kujitazama sisi wenyewe nchi za kiafrika. Maendeleo ya kutegemea hasa nguvu zetu. Kujitegemea kimaendeleo, kujitegemea kiamani na utulivu, kama kazi hii tunayoifanya ya Rwanda na Burundi. Ingekuwa zile zama za zamani, ingebidi tupige kelele tu watu wengine waje watuambie la kufanya. Kwa hiyo, Foundation hii iko kwenye mtazamo sahihi kwa maana kwamba lazima ufike wakati Waafrika mambo yao wafanye wenyewe. Pia pamoja na hilo ni kujitegemea kifikra. Nadhani tuna tatizo kubwa katika Afrika, la watu kutofikiri kwamba katika Afrika tunaweza kujitegemea kifikra. Watu wanafikiri mawazo mazuri lazima yatoke nje ya mipaka yetu. Kwa hiyo nina hakika hii Foundation itatusaidia, itatuelekeza huko kwamba kama tunataka mambo yetu yafanikiwe, sisi wenyewe lazima hata fikra za kutekeleza mambo hayo itoke ndani ya Afrika. Napenda kwa niaba yenu niwashukuru walioweza kubuni Foundation hii. Nimejaribu kutafuta lakini sikuweza kupata hasa hasa ni nani. Hawataki kusema ni Mwalimu, hawataki kusema ni nani, lakini ninasema tunawashukuru wote ambao wameweza kufikiri hili jambo. Mimi nadhani itabidi, kama wengine walivyosema, wa nje nao wawepo ili iwe na mtazamo mpana zaidi. Lakini mimi nadhani sisi Watanzania pamoja na kwamba itakuwa ni Afrika nzima, lakini sisi Watanzania lazima tusimamie, kwa maana kwamba ni fahari ya nchi hii na lazima tuhakikishe inafanikiwa.

Katika nchi zetu hizi za kiAfrika Mwalimu, kama ulivyosema wewe ni mwana siasa katika kundi lile la kwanza katika Afrika. Wako wenzako ambao bado wamo, wengine hawamo, lakini tatizo ambalo tumekuwa tukilipata, wengine tulivyokuwa tunaliangalia, viongozi wetu wakiondoka kwenye madaraka na hata baadaye hata wakiondoka duniani, tunakua na tatizo la kuwazika moja kwa moja na mambo yao yote. Tunawazika na mazuri yote, mara nyingine unaweza kukuta mtu yamebaki yale mabaya, machache mazuri yote tumemzika nayo. Mimi nadhani hii Foundation ni mfano mzuri sana angalau wa kuhakikisha kwamba Mwalimu ukumbusho wako utadumu katika Afrika, si kwa kukumbukwa

tu katika picha lakini kwa kuona kuna kituo kitakachotenda yale uliyokuwa unasimamia katika uhai wako. Kwa kweli mimi nashukuru sana wale ambao wamebuni hili. Kwa kweli ni kitu muhimu sana – mawazo haya mazuri, kazi nzuri aliyofanya Mwalimu katika maisha yake. Ndio maana nadhani uliulizwa pale kwamba ulipotoka urais na sasa huko mbele tena umekutana na vikwazo. Mwalimu hakutoka urais kwa kukimbia matatizo, alijua Afrika ina matatizo mengi na angeliweza kwenda Ulaya akakaa kwa raha, lakini akaona abaki Afrika na Tanzania. Mimi nafikiri ni baraka kubwa sana kwa Tanzania kuwa na Mwalimu. Na ni nafasi yetu nzuri kuonyesha dunia kwamba Foundation si za matajiri tu wa Ulaya na ndizo zinaishi. Hata sisi tuwe na Foundation za kukumbuka watu wetu ambao wamefanya mambo makubwa kuliko wale ambao wamebakiza utajiri duniani.

Baada ya hayo, Mwalimu, nakushukuru sana, nakutakia kila la heri kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wote ambao wamekuja kukusikiliza. Tunakutakia mafanikio katika mambo yote. Mafanikio yako nataka kukuhakikishia ni yetu wote. Ukifanikiwa katika hili la Burundi ni mafanikio yetu wote. Hili la Foundation utafanikiwa, ni mafanikio ya Tanzania. Baada ya hayo nakutakia safari njema. Asante sana kwa mambo yote.